JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MAELEZO YA MHESHIMIWA GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB), WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS,TAMISEMI KATIKA SHEREHE YA UFUNGUZI WA MIUNDOMBINU NA UTOAJI WA HUDUMA YA MPITO YA MRADI WA MABASI YAENDAYO HARAKA (DART) KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM ENEO LA KITUO KIKUU CHA MABASI KARIAKOO GEREZANI TAREHE 25 JANUARI, 2017

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Mheshimiwa Profesa Makame M. Mbarawa (Mb), Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano;

Waheshimiwa Mawaziri mliopo;

Bibi. Bella Bird, Mwakilishi Mkazi wa Benki ya Dunia Tanzania, Burundi, Malawi na Somalia;

Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya kudumu ya Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa;

Katibu Mkuu Kiongozi

Mheshimiwa Paul Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Watendaji Wakuu wa DART na TANROADS;

Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Waheshimiwa Wabunge mliopo;

Makatibu Wakuu mliopo;

Prof. David Mfinanga, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa DART;

Wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Wakala wa DART;

Waheshimiwa Mameya wa Jiji la Dar es Salaam;

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam;

Wakuu wa Wilaya;

Viongozi wa Serikali mliopo hapa;

Viongozi wa Dini mliopo;

Viongozi wa vyama vya siasa mliopo;

Ndugu Wananchi, Mabibi na Mabwana.

Itifaki imezingatiwa.

Mheshimiwa Rais,

1. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa Afya na uzima pia kutupa fursa hii ya kukutana katika tukio hili la kihistoria la ufunguzi wa utoaji wa huduma ya usafiri wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) katika Jiji la Dar es salaam.

   Kwa namna ya pekee na kwa heshima na taadhima naomba kukushukuru wewe Mheshimiwa Rais kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi na kutupa heshima ya kipekee katika sherehe hii ya ufunguzi wa miundombinu na utoaji wa huduma ya mpito ya mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (BRT). Tumefarijika na karibu sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Rais,

2. Utoaji wa huduma za mpito za mabasi ya DART ulianza tarehe 10 Mei, 2016 kama alivyosema Mtendaji Mkuu wa DART na tangu hapo wananchi wanaendelea kunufaika na huduma hiyo ambapo baadhi ya wananchi waliokuwa wanatumia usafiri binafsi, sasa wanatumia usafiri wa umma

na hivyo kuchangia kupunguza msongamano wa magari barabarani na hivyo, imesaidia Wananchi kuwahi katika shughuli zao na kwa upande wa wanafunzi, usafiri huu umewaepusha na adha ya kunyanyaswa katika vyombo vya usafiri. *Kwa sasa wananchi wanaoishi maeneo ya kimara wanatumia kati ya dakika 30 - 40 kufika Ferry tofauti na zamani ambapo walitumia zaidi ya masaa mawili.*

Takwimu zinaonyesha kuwa kila siku kuna upotevu wa zaidi ya Shilingi Billioni 4 katika uchumi wa Mkoa wa Dar es Salaam unaotokana na msongamano wa magari.

Mheshimiwa Rais,

3. Mradi umefanikiwa kutoa ajira 962 zikihusisha madereva, wahudumu wa vituo, usafi, walinzi, wahandisi, mafundi, wahasibu na wasimamizi; kumetokea pia fursa za kibiashara kwa wananchi kama vile huduma ya kuegesha magari karibu na maeneo ya mfumo na biashara zingine ndogo ndogo ambazo ni halali; mfumo umezingatia utoaji huduma kwa abiria wenye ulemavu, wajawazito, wazee na wanafunzi.

Pamoja na hayo, mfumo huu umechangia pia kuboresha mandhari ya Jiji la Dar es Salaam.

Mradi utachangia pia kuinuia hali ya maisha ya wananchi wetu kwani wataweza kuwahi kufika katika maeneo yao ya shughuli za kiuchumi na kijamii na kurudi makwao kwa wakati. Kwa ujumla haya yote yanafanya usafiri huu uwe kichocheo kikubwa cha kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja pamoja na uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Rais,

4. Kama alivyoeleza Mtendaji Mkuu wa DART, tukio hili la leo ni la kihistoria. Kimsingi linajenga taswira na mustakabali mpya katika utoaji wa huduma za usafiri wa umma na wa kisasa. Katika kuhakikisha kuwa mradi huu unaanza kama ulivyopangwa, jitihada kubwa zimefanyika kupitia wadau mbalimbali ambao ni;- OR - TAMISEMI, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wakala wa Barabara (TANROADS), Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), SUMATRA, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, Kampuni ya UDART pamoja na NMB, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kikosi cha

Usalama Barabarani, Mkandarasi STRABAG, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri za Manispaa za Ilala, Ubungo, Temeke na Kinondoni. Ushirikiano wetu umechangia sana kuwezesha huduma hii kuanza pamoja na changamoto zilizokuwa zinaukabili mradi.

Mheshimiwa Rais,

Katika kipindi hiki cha mpito Mtoa huduma ya mpito UDART na Wadau wa Usafiri wa Umma tutaendelea kushirikiana katika kutatua changamoto zote zitakazojitokeza na kujenga uwezo wa kiutendaji na uwajibikaji wa pamoja ili huduma hii iweze kuwanufaisha wananchi wa Jiji la Dar es Salaam na watanzania wote kwa ujumla. Aidha, ikumbukwe kuwa mradi kama huu ni wa kwanza katika ukanda wa Afrika Mashariki. Hivyo tunapaswa kujivunia na kuulinda!

Napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kusimamia kwa karibu na kuhakikisha huduma ya mabasi inaanza wakati mradi ulipokuwa umekwama kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza.

Mheshimiwa Rais,

5. Baada ya maelezo haya sasa kwa mujibu wa ratiba ninaomba kumkaribisha Mheshimiwa Profesa Makame M. Mbarawa (Mb), Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kutoa maelezo na hatimaye kukukaribisha rasmi Mheshimiwa Rais ili uweze kutufungulia rasmi miundombinu na utoaji wa huduma ya mpito ya mradi wa mabasi yaendayo haraka.

Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Karibu Sana.